

KSh. 3,000

**UANUWAI WA KIMOFOLAJIA KATIKA TAFSIRI ZA NOMINO ZA  
PEKEE KATIKA BIBLIA**

**MWANGI SIMON KIARIE**

**C50/CE/2011/2014**

**TASNIFU HII INAWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI ILI  
KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI**

**KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**



Kiarie, Mwangi Simon  
*Uanuwai wa kimofolajia  
katika tafsiri za nomino*



**JUNI, 2023**

**KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY**


UNGAMO

Tasnifu hii ya utafiti ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni yoyote katika chuo kikuu kingine.

MTAFITI

MWANGI SIMON KIARIE

C50/CE/2011/2014



20/06/2023

SAHIHI

TAREHE

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

DKT. LEONARD CHACHA

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA



20/06/2023


SAHIHI

TAREHE

DKT. MIRIAM OSORE

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA



20/06/2023

SAHIHI

TAREHE

**IKISIRI**

Utafiti huu ulinua kuchunguza uanuwai wa kimofolojia katika tafsiri za nomino za pekee katika Biblia tofauti. Biblia zilizofanyiwa utafiti ni *Biblia Habari Njema* na *Biblia Maandiko Matakatifu*. Utafiti huu ulilenga kutathmini mbinu za kutafsiri majina zilizotumiwa katika Biblia, kubainisha maumbo ya kifonolojia na kimofolojia ya majina na vitabu katika Biblia za Kiswahili na kutathmini pengo la kifonolojia na kimofolojia katika majina yaliyotafsiriwa katika Biblia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili kuu: Nadharia ya Vitendo (Skopos) iliyoasisiwa na Reiß na Vermeer (2013) na ile ya Mofolojia Leksia iliyoasisiwa na Katamba (1993). Reiß na Vermeer (2013) wanaeleza kuwa kila tafsiri huwa na nia (Skopos) yake. Lengo la tafsiri ni kuwasilisha matini kwa njia inayoeleweka. Reiß na Vermeer (2013) wanasisitiza umuhimu wa kuhusisha utamaduni wa jamii katika tafsiri. Nadharia ya Mofolojia Leksia huchunguza mwingiliano wa kifonolojia na kimofolojia katika taratibu za ujenzi wa leksimu za lugha fulani. Biblia zilizofanyiwa utafiti ziliteuliwa kwa kutumia usampulishaji kusudi. Data ya majina ya kufanyiwa utafiti ilitoka kwa Biblia hizi mbili. Utafiti huu kimsingi ulifanyiwa maktabani kwa kusoma Biblia na kudondoa majina. Adha, mtafiti alisoma machapisho, vitabu, majarida, mtandao na tasnifu tofauti kisha kuchanganua data husika kwa njia ya majedwali. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kimaelezo.